



**UTT ASSET MANAGEMENT AND  
INVESTOR SERVICES PLC (UTT AMIS)**

**ANNUAL REPORT FOR  
UMOJA UNIT TRUST SCHEME  
(UMOJA FUND)**



**FOR THE YEAR ENDED  
30 JUNE 2024**

## TABLE OF CONTENTS

1.	Timetable and Agenda Items .....	ii
2.	Minutes of the 15 <sup>th</sup> Annual General Meeting.....	1
3.	Matters Arising from the 15 <sup>th</sup> Annual General Meeting .....	19
4.	Chairman's Statement .....	22
5.	Statement of the Custodian .....	26
6.	Report of the Independent Auditors .....	28
7.	Report of the Audited Financial Statements .....	31
8.	Manager's Report .....	36
9.	UTT AMIS News Bulletin .....	43



## UTT ASSET MANAGEMENT AND INVESTOR SERVICES PLC (UTT AMIS)



ANNUAL GENERAL MEETING FOR UMOJA UNIT TRUST SCHEME,  
ON FRIDAY, NOVEMBER 15, 2024 AT THE JULIUS NYERERE  
INTERNATIONAL CONVENTION CENTRE, STARTING AT 8:30AM

### TIMETABLE AND AGENDA ITEMS

S/N	TIME	ACTIVITIES	RESPONSIBLE PERSON(S)
1.	08.30 - 08.45	Arrival and Registration of Investors	Investors / Administration
2.	08.45 - 09.00	Announcements and other Administrative Matters	MC / Administration
3	09.00 - 09.05	Confirmation of Quorum and Opening of the Meeting	Board Chairman
4.	09.05 - 09.20	Introduction of Directors, Management and Service Providers	Managing Director
5.	09.20 - 09.30	Confirmation of Minutes of the 15 <sup>th</sup> Annual General Meeting	All
6.	09.30 - 09.45	Matters Arising from the 15 <sup>th</sup> Annual General Meeting	Managing Director
7.	09.45 - 10.00	Chairman's Statement	Board Chairman
8.	10.00 - 10.30	Presentation of Annual Reports:- <ol style="list-style-type: none"><li>1. Statement of the Custodian</li><li>2. Report of the Independent Auditors on the Summary of Financial Statements</li><li>3. Report on the Audited Financial Statements</li></ol>	CRDB KPMG Director of Finance and Planning
9.	10.30 - 11.00	Presentation of Manager's Report on Investments	Director of Investment and Property Management
10.	11.00 - 11.35	Comments, Questions and Answers Session	Board Members / Management
11.	11.35 - 11.45	Closing of the Meeting	Board Chairman

2

Minutes of the  
15<sup>th</sup> Annual  
General Meeting

**KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA KUMI  
MKUTANO WA KUMI NA TANO (15) WA MFUKO  
WA UMOJA ULIOFANYIKA JUMAMOSI YA  
TAREHE 18 NOVEMBA 2023 KATIKA UKUMBI  
WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS  
NYERERE, DAR ES SALAAM.**



### **WALIOHUDHURIA (Kiambatisho “A”)**

#### **BODI YA WAKURUGENZI**

- |                            |                       |
|----------------------------|-----------------------|
| 1. Bw. Casmir S. Kyuki     | - Mwenyekiti wa Bodi  |
| 2. Dkt. Judika L. King'ori | - Mkurugenzi wa Bodi  |
| 3. Bw. David E. Mwankenja  | - Mkurugenzi wa Bodi  |
| 4. Bw. Paul A. Maganga     | - Mkurugenzi wa Bodi  |
| 5. Bi. Neema J. Jones      | - Mkurugenzi wa Bodi  |
| 6. Bw. Simon M. Migangala  | - Mkurugenzi Mtendaji |

#### **WAJUMBE WA KAMATI ZA BODI YA WAKURUGENZI**

- |                            |                            |
|----------------------------|----------------------------|
| 1. Dkt. Fortunatus Magambo | - Mjumbe wa Kamati ya Bodi |
| 2. Bw. Daniel Olesumayan   | - Mjumbe wa Kamati ya Bodi |

#### **WASIO HUDHURIA KWA TAARIFA**

- |                      |                            |
|----------------------|----------------------------|
| 1. Bw. Lameck Kakulu | - Mjumbe wa Kamati ya Bodi |
|----------------------|----------------------------|

#### **WAALIKWA**

- |                        |  |
|------------------------|--|
| 1. Bw. Vicent. Onjala  | - KPMG/Wakaguzi wa Hesabu za Mfuko             |
| 2. Bi. Rashidah Rashid | - KPMG/Wakaguzi wa Hesabu za Mfuko             |
| 3. Bw. Hemedi Masumai  | - CRDB/Waangalizi wa Mfuko                     |
| 4. Bi. Mariam Mtunguja | - CMSA/ Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana |
| 5. Bi. Anna Gabriel    | - CMSA/ Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana |
| 6. Bw. Josephat Masaba | - Mwakilishi wa Msajili wa Hazina              |

#### **MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS**

- |                        |                     |
|------------------------|---------------------|
| 1. Bw. I. Wahichinenda | 6. Bi. T. Mpiluka   |
| 2. Bw. D. Mbaga        | 7. Bw. R. Mwanga    |
| 3. Bw. S. Bujiku       | 8. Bw. M. Kimario   |
| 4. Bw. S. Kaniki       | 9. Bi. J. Swai      |
| 5. Bi. S. Mgaya        | 10. Bw. P. Ndunguru |

## **1.0 AKIDI NA KUFUNGUA MKUTANO**

Mwenyekiti alifungua mkutano saa 3:05 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe walioweza kuhudhuria Mkutano wa 15 wa Mfuko wa Umoja. Hii ilikuwa baada ya wajumbe kupata taarifa ya akidi, ambayo ilionyesha kwamba Wajumbe wa Mkutano waliohudhuria walikuwa 719 kati ya 107,432 (majina yao yameambatanishwa kwenye Kumbukumbu hizi kama Kiambatisho "A"). Idadi ya vipande vilivyowakilishwa ilikuwa **244,533,538** kati ya jumla ya vipande **345,331,409**. Vipande vilivyowakilishwa ni sawa na asilimia Sabini na moja (71%) ya jumla ya vipande vyote vya Mfuko, na hivyo Mkutano ungeweza kuanza kwa sababu idadi inayohitajika kulingana na Waraka wa Makubaliano (Deed of Trust) ni asilimia kumi (10).

## **2.0 DONDOD/AJENDA ZA MKUTANO**

1. Akidi na Kufungua Mkutano
2. Utambulisho
3. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Uliopita
4. Yatokanayo na Kumbukumbu za Mkutano Uliopita
5. Taarifa ya Mwenyekiti
6. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko
7. Taarifa ya Mkaguzi wa Mfuko
8. Taarifa ya Hesabu za Mfuko
9. Taarifa ya Meneja wa Mfuko Kuhusu Uwekezaji
10. Kipindi cha Maswali na Majibu
11. Kufunga Mkutano

## **3.0 UTAMBULISHO**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwatambulisha Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS, Wajumbe wa kamati za Bodi na Wawakilishi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA). Aliendelea kwa kuwatambulisha Mwakilishi wa Benki ya CRDB ambayo ni Mwangalizi wa Mfuko, Wawakilishi wa Kampuni ya KPMG inayotoa Huduma za Ugaguzi wa Hesabu za Mfuko pamoja na Mwakilishi kutoka ofisi ya Hazina ambayo inasimamia taasisi za serikali. Mkurugenzi Mtendaji alimalizia kwa kutambulisha Menejimenti ya UTT AMIS Pamoja na wafanyakazi wote waliokuwepo Mkutanoni.

## **4.0 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO ULIOPITA**

Baada ya kupitia kumbukumbu ukurasa kwa ukurasa za mkutano wa Kumi na nne (14) uliofanyika tarehe 18 Novemba, 2022, Wajumbe wote walipitisha na kuuthibitisha mhutasari kama kumbukumbu rasmi za Mkutano huo.

## **5.0 YATOKANAYO NA MUHTASARI WA MKUTANO ULIOPITA**

### **5.1 Matumizi ya Teknolojia katika ushiriki wa mkutano kwa njia ya video**

Taarifa ilitolewa kwamba suala la ushiriki wa mkutano kwa kutumia teknolojia kwa njia ya video limetekelezwa. Wawekezaji sasa waliwezeshwa kuhudhuria mkutano ki electroniki popote walipo kwa kutumia simu za mkononi au tarakilishi kupitia linki zilizosambazwa kwa njia ya meseji, kwenye tovuti ya UTT AMIS na mitandao ya kijamii ya UTT AMIS.

## **6.0 TAARIFA YA MWENYEKITI**

Mwenyekiti aliwasilisha taarifa yake kuhusu Mfuko wa Umoja kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Taarifa hiyo ilikuwa kama ifuatavyo: -

- 6.1 Taarifa ilieleza kwamba katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 30 2023, utendaji wa mfuko uliendelea kuwa mzuri. Faida ya wawekezaji kwa mwaka ilikuwa kubwa kulinganishwa na Kigezo Linganifu. Faida ya mwaka ilikuwa asilimia 11.2 ikilinganishwa na asilimia 7.6 ya Kigezo Linganifu ambapo katika kipindi cha mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2023 thamani ya Mfuko iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 289.0 tarehe 30 Juni 2022 hadi Shilingi bilioni 320.0 tarehe 30 Juni 2023. Ongezeko la thamani ya Mfuko linatokana na imani ya Wawekezaji pamoja na kueleweka kwa elimu iliyotolewa kuhusu faida za mifuko ya uwekezaji wa pamoja.
- 6.2 Kuhusu mwenendo wa uchumi na mazingira katika masoko ya fedha, ilielezwa kuwa wakati Dunia inazidi kupata ahueni juu ya athari za UVIKO 19 na madhara ya vita nchini Ukraine, hali ya uchumi, imeendelea kuimarika na kukua kwa asilimia 4.7 kwa mwaka 2022 na kiwango cha asilimia 5.4 na silimia 5.2 kwa robo ya kwanza naya pili kwa mwaka 2023. Uchumi wa Tanzania umekuwa ni zaidi ya ukuaji katika nchi za ukanda wa Jagwa la sahara na nchi za ukanda wa ushirikiano wa mandeleo kusini mwa Afrika (SADC) ambao ni asilimia 3.5. Mfumuko wa bei ulikua asilimia 4.0 kwa mujibu wa tarifa ya benki kuu ya Tanzania, ya kipindi cha robo mwaka ilioshia tarehe 30 Juni 2023, pia thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya marekani ilipungua kidogo kwa kiwango cha asilimia 1.0 na kuongezeka thamani dhidi ya fedha za baadhi ya nchi za Africa Mashariki kwa viwango vya hadi asilimia 15.0.
- 6.3 Kwa upande wa soko la mitaji na dhamana, ilielezwa kuwa kumekuwa na ongezeko katika bei za hisa. Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Kwa mujibu wa fahrisi, imeonyesha kuwa na ongezeko la asilimia 4.1 kutoka 3,928.54 tarehe 30 Juni 2022 hadi

- 4,091.8 tarehe 30 Juni 2023 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 7.5 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Hii inamaanisha kwamba katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2023, bei za hisa kwa ujumala ziliongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita.
- 6.4 Sababu zilizopelekea kupanda kwa bei za hisa, ziliezwa kuwa ni pamoja na utendaji mzuri wa makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, kuongezeka kwa imani ya wawekezaji ndani na nje ya nchi na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji hapa nchini. Shukuranzi zilitolewa kwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali kwa ujumla kwa kuweka sera na mazingira bora ya biashara na uwekezaji.
- 6.5 Kuhusu ukuaji wa Mifuko inayoendeshwa na Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS, taarifa inaonyesha kuwa kwa Mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023, thamani ya mifuko iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 996.5 iliofikiwa tarehe 30 Juni 2022 hadi kufikia Shilingi Triliioni 1.535 tarehe 30 Juni 2023 ongezeko la shilingi bilioni 538.9, sawa na asilimia 54.0 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi billioni 383.7, sawa na asilimia 62.6 kwa mwaka ulioishia June 30, 2022. Ongezeko la ukubwa wa Mifuko, limetokana na ongezeko la idadi ya wawekezaji 47,480, sawa na asilimia 24 waliojunga katika Mifuko kwa mwaka 2023 ikilinganisha na wawekezaji 29,832, sawa na asilimia 17 waliojunga mwaka wa fedha uliotangulia.
- 6.6 Illobainishwa kuwa Kampuni ya UTT AMIS inaendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa miaka mitano (5) utakaoishia mwezi Juni mwaka 2024. Katika Mpango Mkakati huo Kampuni imeazimia kujikita kwenye matumizi ya teknolojia katika kutoa huduma kwa wawekezaji. Katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2023, UTT AMIS imekamilisha uunganishaji wa mifumo yake na mifumo ya Benki za NMB, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) na Benki ya Stanbic. Aidha, UTT AMIS imeendelea na miradi ya kuunganisha mifumo yake na mifumo ya Benki ya EXIM, Benki ya Absa, Benki ya KCB, Benki ya watu wa Zanzibar, Benki ya DCB na Benki ya UBA ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Pindi miradi hii itakapokamilika, miamala ya kidigitali, ambayo sasa ni asilimia 70 itaongezeka na kufikia asilimia ya juu zaidi.
- 6.7 Matarajio kwa kipindi cha miaka minne ya utendaji wa Mpango Mkakati wa Kampuni ya UTT AMIS unaoishia Juni 2024 kumekuwa na mafanikio makubwa zaidi ya ilivytarajiwa. UTT AMIS ikiwa imebakiwa na mwaka mmoja wa utekelezaji wa mpango mkakati huo,
- imeshaanza kuandaa mpango mkakati mpya wa miaka mitano, ikiwemo kuboresha mifumo na huduma kwa wawekezaji pamoja na kubainisha fursa nyingine za kibiaresha kwa manufaa ya wawekezaji, serikali Pamoja na wadau wengine.
- 6.8 Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, alimalizia kuwasilisha taarifa yake kwa kutoa shukranzi zake za dhati kwa wadau wote walioshirikiana na Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS na Mifuko wa Umoja kwa kipindi chote cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Kwa namna ya kipekee shukuranizilitolewa kwa Serikali kuitia Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Msimamizi wa Mifuko ambaye ni Benki ya CRDB, Soko la Hisa la Dar es Salaam pamoja na Madalali wake, Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, Wafanyakazi wa UTT AMIS na Wadau wote ambao wameendelea kuiwezesha UTT AMIS kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha.

## 7.0 TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO

- 7.1 Mwakilishi wa Benki ya CRDB ambayo ni Mwangalizi wa Mfuko wa Umoja, aliwasilisha Taarifa kwamba jukumu lao kama Waangalizi wa Mfuko wa Umoja ni kusimamia utendaji wa meneja wa mfuko kunaendana na waraka wa makubaliano (Deed of Trust) ili kuhakikisha maslahi bora ya wawekezaji katika Mfuko. Mwakilishi alielezea kuwa katika utekelezaji wa kazi hiyo, Mwangalizi wa mfuko ana majukumu makuu matatu ambayo ni; Uangalizi wa mali za mfuko, kuhakikisha meneja wa mfuko anatumia njia/mbinu sahihi katika kukokotoa mahesabu ya thamani ya mfuko sambamba na mkatuba wa makubaliano (Deed of Trust) na pia kuhakikisha viwango vya uwekezaji vinazingatiwa.
- 7.2 Mwakilishi wa Benki ya CRDB alieleza kwamba katika kipindi cha mwaka wa fedha kilichoanza tarehe 01.07.2022 mpaka 30.06.2023, Benki ya CRDB kama mwangalizi wa mfuko wa Umoja, wameedeleza uangalizi wa mwenendo wa shughuli za Meneja wa mfuko na utekelezaji wake Pamoja na changamoto kwenye uwekezaji.
- 7.3 Mwakilishi alihitimisha kwa kuwathibitishia wawekezaji kwamba shughuli za uwekezaji kwenye mfuko wa Umoja na wajibu wa meneja wa mfuko (UTT AMIS) vimeendeshwa kufuatana na vipengele vya waraka wa makubaliano, wakizingatia suala la uaminifu wa wenyе vipande kwenye mfuko, walithibitishia kwamba maslahi ya wenyе vipande ndani ya mfuko wa Umoja yalilindwa na kuzingatiwa ipasavyo na meneja ameendesha mfuko kulingana na waraka wa makubaliano.

## **8.0 TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MFUKO WA UMOJA**

- 8.1 Mwakilishi kutoka Shirika la Wahasibu la KPMG ambao ni Wakaguzi wa Mfuko aliwasilisha muhtasari wa taarifa kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Mfuko wa Umoja kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Alieleza kuwa Muhtasari wa taarifa ya Hesabu za Mfuko zilizowasilishwa yaani Taarifa ya Mapato na Matumizi, Urari wa Hesabu za Mfuko, Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko na Taarifa ya Mtiririko wa Fedha umetayarishwa kutoka katika taarifa kamili ya ukaguzi wa Mfuko wa Umoja kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023.
- 8.2 Taarifa ilielezea kuwa muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha hauoneshi taarifa zote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha (International Financial Reporting Standards (IFRS) na kwamba muhtasari wa hesabu za kifedha zilizokaguliwa siyo mbadala wa taarifa kamili za hesabu zilizokaguliwa na hajumuishi matukio au miamala baada ya tarehe za taarifa ya hesabu za kifedha zilzokaguliwa.
- 8.3 Pia taarifa ilielezea maoni ya ukaguzi (audit opinion) yasiyokuwa na kasoro juu ya taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za kifedha za Mfuko yaliyotolewa kwenye taarifa tarehe 11 Novemba 2023 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023 na inajumuisha mambo mengine muhimu juu ya ukaguzi wa hesabu za mfuko.
- 8.4 Mwakilishi huyo alihitimisha taarifa yake kwa kueleza kuwa majukumu yao kama wakaguzi wa hesabu za mfuko ni kutoa maoni kama muhtasari wa hesabu za Mfuko unaendana na taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha na kwa mujibu wa taratibu zao za ukaguzi, ukaguzi ambao ulifanywa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi (International Standards on Auditing). Alihitimisha kwa kusema mfuko uliweza kupata Hati safi ya Ukaguzi.

## **9.0 TAARIFA YA MWAKA KUHUSU HESABU ZA MFUKO WA UMOJA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI 2023**

- 9.1 Mkurugenzi wa Fedha na Mipango wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwasilisha Taarifa ya Hesabu za Mfuko wa Umoja katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Mkurugenzi aliwaomba wawekezaji kusoma taarifa kwa kulinganisha hali ya utendaji ya mfuko kwa mwaka uliopita 2022.
- 9.2 Alieleza kuwa taarifa hiyo imegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni, Taarifa ya Mapato

na Matumizi, Urari wa Hesabu za Mfuko, Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko na Taarifa ya Mtiririko wa Fedha.

- 9.3 Kwa upande wa Mapato na Matumizi, Jumla ya Mapato yalikuwa ni shilingi 41,065,388,000/= ukilingaisha na kiasi cha shilingi 41,859,516,000 kwa mwaka uliopita 2022. Gharama za uendeshaji zilikuwa shilingi 7,946,706,000/= ukilinganisha na shilingi 7,452,007,000 kwa mwaka 2022. Mapato kabla ya kodi ilikuwa shilingi 33,118,682,000/= mwaka 2023 ukilinganisha na shilingi 34,407,509,000/= mwaka uliopita 2022. kodi ya zuijilikuwa ni shilingi 320,218,000/= mwaka 2023 ukilinganisha na shilingi 295,234,000/= mwaka uliopita 2022. Mapato halisi baada ya kodi mwaka 2023 yalikuwa shilingi 32,798,464,000/= ukilinganisha na shilingi 34,112,275,000/= mwaka uliopita 2022.

9.4 Kwa upande wa Urari wa Hesabu za Mfuko ilielezea kuwa Rasilimali za Mfuko mwaka 2023 zilikuwa shilingi 327,734,824,000/= ukilinganisha na kiasi cha shilingi 295,220,313,000/= kwa mwaka wa fedha uliopita 2022 . Pia jumla ya Dhima ya mfuko kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023 ilikuwa ni shilingi 2,304,985,000/= ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita 2022 dhima ilikuwa ni shilingi 1,874,494,000/= hivyo kufanya thamani halisi ya Mfuko mnamo tarehe 30 Juni 2023 kuwa shilingi 325,429,839,000/= ukilinganisha na kiasi cha shilingi 293,345,819,000/= mwaka uliopita 2022.

- 9.5 Katika taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko ileezwa kuwa, thamani ya mfuko mwanzoni wa mwaka ulioanza tarehe 1 Julai 2023 ilikuwa shilingi 293,345,819,000/= ukilinganisha na mwaka uliopita 2022 ambapo ilikuwa ni shilingi 261,508,198,000/. Ongezeko la mabadiliko ya thamani ya mfuko ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023 ilikuwa ni shilingi 32,798,464,000/= ukilinganisha na mwaka uliopita ilikuwa ni shilingi 34,112,275,000/=. kadharika Miamala ya wenye vipande zililipwa (Net repurchase) ya kiasi cha shilingi 714,444,000 mwaka 2023 ikilinganishwa na malipo (Net repurchase) ya shilingi 2,274,654,000 kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022 hivyo imepelekeea mabadiliko ya thamani halisi ya Mfuko kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023 kuwa shilingi 325,429,839,000/= ukilinganisha na mwaka 2022 thamani halisi ya Mfuko ilikuwa ni shilingi 293,345,819,000/=.

9.6 Kwa upande wa Taarifa ya Mtiririko wa Fedha, ilielezea kuwa fedha halisi kabla ya marekebisho ya mtaji wa uendeshaji ilitumika shilingi

111,981,000/= ikilinganishwa na matumizi ya shilingi 1,676,827,000/= mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Vile vile ilielezwa kuwa Fedha iliyopatikana kutoka kwenye shughuli za uendeshaji baada ya marekebisho ya mtaji na Kodi ya Serikali ilikuwa shilingi 876,790,000/=kwa mwaka ulioishia Juni 2023 ikilinganishwa na matumizi ya kiasi cha shilingi 6,112,914,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Malipo ya amana kwa wawekezaji hadi 30 Juni 2023 yalikuwa shilingi 714,444,000/= ikilinganishwa na shilingi 2,274,654,000/= kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2022. Miamala hiyo imapelekeea ongezeko la fedha kiasi cha shillingi 162,346,000/= katika Mwaka wa fedha ulioshia 30 Juni 2023 ukilinganisha na Matumizi (Net outflows) ya shillingi 8,387,568,000/= 30 Juni 2022. Aidha Mfuko ulikuwa na akiba ya Fedha kiasi cha shilingi 442,758,000/= Mwanzioni mwa mwaka wa fedha 2023 ikilinganishwa na akiba ya shilingi 8,830,326,000/= Mwanzioni mwa Mwaka wa Fedha 2022, hivyo kupelekeea Mfuko kubaki na akiba ya fedha taslimu kiasi cha shilingi 605,104,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023 ikilinganishwa na shilingi 442,758,000/= mwishoni mwaka wa fedha 2022.

## **10.0 TAARIFA YA MENEJA WA MFUKO KUHUSU UWEKEZAJI**

- 10.1 Mkurugenzi wa Idara ya Uwekezaji ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwasilisha Taarifa ya Meneja kuhusu uwekezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni,2023.
- 10.2 Taarifa ilieleza kuwa ukubwa wa Mfuko wa Umoja uliongezeka kwa Shilingi bilioni 31.0 katika mwaka wa fedha unoisha tarehe 30 Juni 2023, ukubwa wa Mfuko uliongezeka kwa asilimia 10.7, faida ya mwaka na thamani ya kipande iliongezeka na kufikia Shilingi 926.9 kwa kila kipande kutoka Shilingi 833.6 ilionakiliwa tarehe 30 Juni 2022.
- 10.3 Taarifa iliainisha mgawanyo wa uwekezaji wa Mfuko wa Umoja katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioisha tarehe 30 Juni 2023, Kampuni ya UTT AMIS kama Meneja wa Mfuko alitumia uzoefu na weledi katika kufikia mgawanyo anuai wa rasimali kwa mujibu wa matakwa ya sera za mfuko wa Umoja. Taarifa ilieleza kuwa mgawanyo wa uwekezaji katika Mfuko wa Umoja uligawanyika katika asilimia kama ifuatavyo, asilimia 39.9 iliwekezwa katika hisa, asilimia 52.3 iliwekezwa katika dhamana za serikali za muda mrefu, asilimia 7.3 kwenye hati fungani za Kampuni binafsi, asilimia 0.3 katika amana za benki za muda maalumu na asilimia 0.2 kwenye amana za benki za muda mfupi.
- 10.4 Mkurugenzi wa Idara ya Uwekezaji aliendelea

kuelezea ulinganishi wa faida ya Mfuko wa Umoja na viwango linganishi vyta riba vinavyotolewa na soko kwenye amana za benki. Faida katika Mfuko wa Umoja kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2023 ilikuwa ni asilimia 11.2 ikilinganishwa na faida itokanayo na kigezo cha ufanisi cha asilimia 7.6 (benchmark).

- 10.5 Taarifa ya Meneja ilibainisha mwenendo wa uchumi nchini ambako kwa mwaka 2023 unakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 5.2, ukichangiwa na kufufuliwa kwa shughuli za uchumi hususani uwekezaji kwenye sekta ya umma na binafsi nchini. Hali ya mwenendo wa uchumi nchini iliendelea kuwa imara na stahimilivu ambapo hali hii ni muhimu kwa Mifuko ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa na UTT AMIS. Uchumi imara husaidia kutunza na kuimarisha thamani ya uwekezaji na huvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.
- 10.6 Taarifa iliendelea kuelezea kuhusiana na hali ya Mfumuko wa bei nchini kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023 ni asilimia 3.6 ikilinganishwa na asilimia 4.4 iliyonakiliwa Juni 2022. Kupungua kwa mfumuko wa bei nchini kunaashiria gharama za bidhaa na huduma mbalimbali zilipungua kwa mwaka ulioishia Juni 2023 ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo Juni 2022. Hali ya uchumi nchini na mwenendo wa mfumuko wa bei umeendelea kuwa stahimilivu kiasi ambacho kimevutia wawekezaji kuwekeza kwa wingi. UTT AMIS inajitahidi kuwekeza kwenye maeneo yanayotoa faida shindani kuliko kiwango cha mfumuko wa bei.
- 10.7 Kwa upande wa Sekta ya Benki kwa kipindi cha mwaka kilichoishia Juni 2023 hali ya utendaji kwa sekta ya benki nchini imeendelea kuwa imara kwani jumla ya rasimali na amana ziliongezeka. Ongezeko kwenye rasimali ni Shilingi trillioni 8.0 sawa na asilimia 17.5 kutoka shilingi trillioni 45.7 mwaka 2022 hadi trillioni 53.7 mwaka 2023. Jumla ya amana kwenye benki iliongezeka kwa Shilingi trillioni 5.7 sawa na asilimia 20.3 hadi kufikia Shilingi trillioni 33.7 Juni 2023.
- 10.8 Mwasilishaji alieleza namna sekta ya mawasiliano inavyoendelea kuchochea na kurahisisha Uwekezaji katika mifuko na huduma binafsi. Taarifa iliainisha kuwa kwa kupiga \*150\*82# au kwa kutumia programu tumizi mwekezaji anaweza kufungua akaunti na kuanza Uwekezaji wake. Aidha kupitia simu mwekezaji anaweza kununua na kuuza vipande.
- 10.9 Taarifa ya Meneja ilieleza kwamba kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioishia tarehe 30 Juni 2023, Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania iliongeza kiasi cha dhamana za Serikali za muda mfupi

- sokoni ikilinganishwa na mwaka uliopita ulioishia tarehe 30 Juni 2022 kwa Shilingi triliioni 1.4 sawa na asilimia 73.6 hadi shilingi triliioni 3.3 Juni 2023. Hata hivyo, uhitaji wa dhamana za serikali za muda mfupi uliongezeka kwa asilimia 24.1(shilingi triliioni 0.7) hadi kufikia shilingi triliioni 3.6 kutoka shilingi triliioni 2.9 mwaka jana.
- 10.10 Aidha taarifa iliendelea kuelezea kwamba viwango vya riba katika dhamana za serikali za muda mfupi vilipungua kutoka wastani wa asilimia 3.5 mwezi Juni 2023 kutoka asilimia 4.1 mwaka jana 2022. Aidha viwango vya riba jumuishi za mikopo katika benki ya biashara ni asilimia 16.7 ikilinganishwa na asilimia 16.2 kwa mwaka uliopita. Uwekezaji kwenye amana za benki kwa muda wa mwaka mmoja zilitoa faida ya asilimia 8.2 ikilinganishwa na asilimia 8.0 mwaka 2022.
- 10.11 Katika Viwango vya Kubadilisha Fedha, taarifa ilibainisha kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja kilichoisha mwezi Juni 2023, viwango vya kubadilisha fedha kati ya Shilingi ya Kitanzania na fedha za kigeni vimeendelea kuwa stahimilivu. Thamani ya Shilingi kwa Dola moja ya Kimarekani ilikuwa imara na ya kuridhisha ingawa ilipungua kidogo kwa asilimia 1.0 kutoka Shilingi 2315.7 Juni 2022 hadi Shilingi 2339.1 Juni 2023. Taarifa ilielezea kwamba uimara wa viwango vya kubadilisha fedha ni muhimu kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja na serikali kwa ujumla kwa sababu inasaidia kutunza thamani ya rasilimali ambazo thamani yake ipo katika shilingi za kitanzania na kuvutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya Tanzania.
- 10.12 Katika upande wa Soko la Mitaji na Dhamana kwa kipindi hadi Juni 2023 limekuwa imara na thabiti, kwani limepelekea kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji katika soko la hisa, mitaji, dhamana na kwenye mifuko ya uwekezaji wa Pamoja. Soko limekuwa likifanya kazi nzuri kwa upande wa mauzo na shughuli mbalimbali, tuliona utoaji wa hatifungani mbili mpya za benki ya taifa ya biashara (NBC-Twiga) na benki ya biashara ya kenya (KCB-Fursa Sukuk) zilizofanikiwa kufanya vizuri kwani jumla ya shilingi bilioni 49.9 zilipatikana. Mwezi Novemba 2022 shirika la Watumishi Housing (WHI) lilizindua mifuko wa uwekezaji wa pamoja unaoitwa Mfuko wa Faida (Faida fund) ambao ulifanikiwa kuvutia wawekezaji na hadi Disemba 2022 mfuko ulinakili shilingi bilioni 7.9.
- 10.13 Kuhusu hali ya soko la Hisa, hali ya mauzo ya hisa ilipungua kwa takribani Shilingi bilioni 19.0 sawa na asilimia 15.0 kutoka Shilingi bilioni 126.6 hadi Shilingi bilioni 107.6 tarehe 30 Juni 2023. Vilevile ukubwa wa mtaji wa soko ulipungua thamani kwa Shilingi triliioni 0.6 (asilimia 5.4) hadi shilingi triliioni 15.0 kutoka shilingi triliioni 15.6 Katika kipindi cha mwaka mmoja kampuni sita zilitangaza na kulipa gawio nazo ni; TCC/Sigara (Tsh. 670.0), TPCC (Tsh. 390.0), TBL (Tsh. 290), benki ya NMB (Tsh. 286.0), SWISS (Tsh. 42.0), na benki ya CRDB (Tsh. 45) kwa kila hisa. Hivyo basi, kwa wawekezaji wote waliowekeza kwenye kampuni tajwa walipata gawio sawa na maelezo hapo juu.
- 10.14 Meneja alihitimisha taarifa ya Uwekezaji kwa kuwashakishia wawekezaji wa Mfuko wa Umoja kuwa hadi tarehe 30 Juni 2023 jumla ya rasilimali kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa na Taasisi ya UTT AMIS imefika Shilingi trillion 1,535.4 kutoka Shilingi bilioni 996.5. Rasilimali ziliongezeka kwa asilimia 54.0 sawa na ongezeko la Shilingi bilioni 538.9 ikilinganishwa na ongezeko la Shilingi bilioni 383.7 iliyonakiliwa mwaka uliopita 2022 kwa kipindi chote hadi Juni 2023 kumekuwa na muamko wa uwekezaji kwenye mifuko hali iliyopelekea ongezeko kubwa la rasilimali.
- 10.15 Meneja aliwashakishia wawekezaji kuwa ataendelea kubuni na kuvumbua mianya na fursa za uwekezaji kadiri zinavyojitokeza katika soko ili kuongeza mapato na faida kwa wawekezaji. Lengo likiwa ni kuvuka matarajio ya wawekezaji kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

## 11.0 MASWALI, MAONINA NA MAJIBU

- 11.1 Wawekezaji walikuwa na maswali na maoni yafuatayo:**
- 11.1.1 Mwekezaji alitoa pongezi na shukrani kwa bodi na UTT AMIS kwa ujumla kwa maandalizi mazuri ya mkutano. Alielea kwamba matangazo ya taarifa za mkutano yalitolewa mapema na kwa wingi na taarifa ziliweza kusambaa na kuwafikia wawekezaji kwa wakati. Alishauri kwamba juhudhi za kuitangaza mifuko ya UTT AMIS ziendelee sambamba na uboreshaji wa huduma kwa wateja hasa huduma kwa njia ya simu (call centre) na kuendelea kuwaatamia wawekezaji kwa kuwawekeea mazingira rafiki, kuwajali, kutoa vitu vya ziada (chai, chakula) vya kuwavutia. Pia pongezi nyingi zilitolewa kwa wawekezaji kwa kuhudhuria mkutano kwa wingi.
- 11.1.2 Mwekezaji alihitaji ufanuzi juu ya taarifa ya

- mwenyekiti, hasa kwenye kupungua kwa faida kulinganisha na mwaka jana kutoka asilimia 12.6 mpaka asilimia 11.2
- 11.1.3 Ufafanuzi uliombwa juu ya changamoto zinazomkabili msimamizi wa mfuko CRDB, na wamevezaje kuzikabili
- 11.1.4 Mwekezaji aliomba kufahamu kirefu cha KPMG.
- 11.1.5 Mwekezaji aliomba ufanuzi kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, fedha halisi itokanayo na shughuli za uendeshaji kati ya mwaka wa fedha 2023 na mwaka jana 2022. Na je inamanisha nini hususani kwenye hasara na faida.
- 11.1.6 Mwekezaji alitoa maoni kuhusu kuweza njia bora na rahisi kwenye kuuza vipande vya wawekezaji kama vile ilivyokua kununua.
- 11.1.7 Mwekezaji aliomba kufahamu, Je inawezekana kujua mtiririko wa fedha tangu mwanachama ameanza mwaka 2005 mpaka sasa kwa kutumia menu ya UTT AMIS (\*150\*82#) au kwenye application.
- 11.1.8 Mwekezaji aliomba kupata ufanuzi juu ya Mfuko wa Umoja kubadilishwa kutoka kwenye gawio kwenda kukuza mtaji na jinsi ya kupata faida husika.
- 11.1.9 Mwekezaji alipendekeza uwepo wa chai ya asubuhi kwa wawekezaji kabla ya kuingia kwenye mkutano.
- 11.1.10 Mwekezaji alitoa malalamiko yake juu ya kuchelewa kujibiwa kwa simu ya huduma kwa wateja.
- 11.1.11 Mwekezaji alitoa maoni yakuwepo kwa malengo kwa menejimenti ili mwisho wa mwaka kuweza kujadili kama yamefikiwa au la.
- 11.1.12 Mwekezaji alipendekeza kwamba badala ya wawekezaji kupewa chakula kwenye mkutano wapewe fedha.
- 11.1.13 Mwekezaji alitoa pungezi kwa taasisi kwa kuyafanya kazi mapendekezo mengi ambayo yanatolewa na wawekezaji, pia, aliomba kwamba taasisi iangalie na kuboresha manunuzi ya vipande yaweze kufanyika kwa uharaka na hapo kwa papo.
- 11.1.14 Mapendekezo yalitolewa kwamba picha mbalimbali zinazoendana na mfuko na wawekezaji ziwekwe katika ripoti ili kuipendezesha zaidi.
- 11.1.15 Mwekezaji mwingine alitaka kufahamu, jinsi gani taasisi inawefikia vijana.
- 11.2 Wawakilishi wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS walitoa Majibu na ufanuzi kama ifuatavyo:**
- 11.2.1 Bodi na menejimenti ilipokea pungezi na mapendekezo yaliyotolewa na wawekezaji na kusema kwamba jithada kubwa zinafanywa kuwafikia wawekezaji, pia nguvu kubwa imelekezwa katika kutoa elimu na huduma kwa wawekezaji.
- 11.2.2 Kuhusu suala la kupungua kwa faida kutoka asilimia 12.6 mwaka jana kwenda asilimia 11.2, ilielezwa kuwa hii ni kutokana na ushindani wa masoko na faida na pia kushuka kwa viwango vya riba kwenye dhamana za serikali za uwekezaji.
- 11.2.3 Kuhusu changamoto za wawekezaji zilizokuwepo kwa CRDB, Muakilishi kutoka CRDB alizainisha changamoto ikiwemo uwelewa mdogo wa huduma zinazotolewa na UTT AMIS, kutoa huduma bora na changamoto za kimfumo. Changamoto hizi zinatatuliwa kwa kutoa elimu, Kuboresha huduma na kuboresha mifumo ambayo kwa sasa imeunganishwa moja kwa moja na mifumo ya UTT AMIS.
- 11.2.4 Kuhusu kirefu cha wakaguzi wa Hesabu KPMG maelezo yalitolewa kuwa herufi hizo zinasimama badala ya majina ya waanzilishi wa kampuni hiyo ambao ni Klynveld, Peat, Marwick na Goerdeler.
- 11.2.5 Menejimenti ilieleza kuwa mabadiliko kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha katika mwaka wa fedha na mwaka jana hayana uhusiano na faida ila inaonesha jinsi mtiririko wa fedha wa Taasisi unavyotoka na kuingia.
- 11.2.6 Menejimenti ilipokea maoni ya mwekezaji kuhusu urahisi wa kuuza vipande (repurchase) na kueleza kuwa ipo katika hatua za awali za utekelezaji wa huduma ya wawekezaji kuweza kuuza vipande kwa simu na kwa sasa wawekezaji wanaweza kutoa hadi Milioni 2. Uboreshaji wa huduma hii utandelea.
- 11.2.7 Kuhusu suala la kuweza kupata mtiririko wa fedha kwa mwekezaji tokea alivyoanzisha mfuko 2005, ilielezwa kuwa wawekezaji wanaweza kupata taarifa hiyo muda wowote wanapoitaji.
- 11.2.8 Ilielezwa kwamba mfuko wa Umoja ulibadilishwa kutoka kuwa mfuko wa kutoa gawio kwa mwezi kuwa mfuko wa kkuza mtaji ambapo faida inabaki kwenye akaunti ya mwekezaji na kuendelea kkuza mtaji wake. Hata hivyo, mwekezaji anaruhusiwa kuuza vipande wakati wowote.
- 11.2.9 Kuhusu kuuwepo kwa chai asubuhi kwa wawekezaji kabla ya kikao, pendelezo lilipokelewa na menejimenti iliahidi kulifanya kazi.
- 11.2.10 Menejimenti ilieleza kuwa imefanya kazi swala la mawasiliano kwa wateja na zaidi imeongeza

nguvu kazi kwa kuajiri watu wengi zaidi wa mawasiliano na kuweka mifumo bora ili kuongeza ufanisi kwenye mawasiliano kwa kutoa huduma bora kwa wateja.

11.2.11 Menejimenti ilieleza kwamba malengo ya taasisi yapo na kwamba ipo mwishoni katika kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano ambao umekuwa ukitekelezwa toka mwaka 2019 mpaka mwaka 2024 na kuanza mpango mkakati mwingine wa miaka 5 ambao utekelezaji wake ni kuanzia mwaka 2024 mpaka mwaka 2029. Taasisi inafanya vizuri na malengo yote yaliweza kufikiwa kwa haraka kabla ya muda husika. Iliezwa kuwa kwenye miaka ijayo kutakuwa na kipande kwenye ripoti kinachoeleza mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka husika wa fedha.

11.2.12 Kuhusu kutoa bahasha (Fedha) badala ya chakula, iliezwa kuwa kutoa fedha kwenye mukutano kama mbadala wa chakula cha mchana inaenda kinyume na kanuni na miongozo za mifuko lakini taasisi itaendelea kushauriana namna bora ya kuboresha.

11.2.13 Kuhusu kuwa na uvezakano kwamba vipande vikinunuliwa iweze kuonekana hapo kwa papo, iliezwa kuwa hii ni ngumu kwasababu bei ya kipande inayotumika siku hiyo ni bei inayopatikana mwisho wa siku husika maana masoko huwa yanafungwa jioni na kutoa bei husika ambayo hutumika kwenye kuvibadili vipande husika.

11.2.14 Kuhusu kuweka kumbumbu ya picha kwenye ripoti, maoni yalipokelewa na menejimenti na kuelezwu kuwa itaendelea kuboresha ripoti na inapobidi, kuweka picha

11.2.15 Kuhusu kuwafikia vijana, iliezwa kwa sasaivi vijana ni wengi sana na Taasisi imekuwa ikitembelea vyuoni na kutoa elimu ili kupata wawekezaji vijana. Pia iliezwa kuwa taasisi imeweka nguvu katika kutoa elimu kiujumla ili kuwagusa vijana wengi vyuoni na mtaani.


## 12.0 KUFUNGA MKUTANO

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwashukuru Wawekezaji kwa kuhudhuria Mkutano huo. Pia aliwahakikishia ya kuwa mawazo na mapendekezo waliyoyatoa katika Mkutano yatazingatiwa na yale yanayowezekana yatakelezwa. Mwisho aliwatakia heri ya sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya 2024. Mkutano ulifungwa saa 06.49 Mchana.

**MWENYEKITI**

**KATIBU**

**TAREHE**



## KIAMBATISHO “A”

**OORODHA YA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA UMOJA WALIOHUDHURIA  
KWENYE MKUTANO MKUU ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA  
KIMATAIFA JULIUS NYERERE, DAR ES SALAAM TAREHE 18 NOVEMBA 2023**

S/N	JINA LA MUWEKEZAJI
1	AARON ERNEST MLAKI
2	ABDALLA ZUBERI SEMKUYA
3	ABDALLAH AMIRI MCHOMVU
4	ABDALLAH FUNDI KAWAMBWA
5	ABDALLAH MPALUPALU JUMA
6	ABDALLAH SAID BUNGA
7	ABDUL ALLY MFUNDILI
8	ABDULKARIM HASSAN MNACHO
9	ABDULRAHIM ALLY BARUAN
10	ABEID MUSTAFA MAWAKA
11	ABUBAKAR JABU NYUNDO
12	ADAH MDESA MWASHA
13	ADAM KIMWERI NYELLO
14	ADELIN BENEDICT TOSSI
15	ADELINA JOHN XSAXIER
16	ADIL HAMDUN SEIF
17	ADRIAN JOACHIM MAKELELE
18	AGNELUS FROLIAN MWITUMBA
19	AGNES BERNARD MASSAWE
20	AGNES PEREGRIN MAKONDE
21	AGNES PHILIP NYAGILO
22	AGNESI FRANCIS MAENDAENDA
23	AGNESS JOSEPH KITUNDU
24	AGNESS PETER JABE
25	AIEKA ELIKALIA MACHA
26	AINEA NDEKARISHO KISHIMBO
27	AISHA RAMADHANI KAPANDE
28	AKIDA RAMADHAN MWAIMU
29	ALBANUS BLASS NJAU
30	ALBERT HENRY MBOTTO
31	ALEX WATSON KASUNGA
32	ALICK SAMWEL MWANGOKA
33	ALIKO JOHN MWANEMILE
34	ALLAN LUCA MWAIGAGA
35	ALLY ABDALLAH HENG
36	ALLY AMIRI MKWIZU
37	ALLY HASSANI MALYELYE
38	ALLY JUMA KHAMIS

39	ALLY MARO MACHOTA
40	ALOISIA MARY ALOYCE LEKULE
41	ALOYCE LEMS KIWANGA
42	ALPHONCE JOSEPH MABULA
43	ALPHONCE PETRO BAHEMKE
44	ALUMBWAGE ELLY MUNGONGO
45	AMAN BAKARI LIWALI
46	AMINA ABEID DAUDA
47	AMINA MNINGO NGUDE
48	AMINA MWINYI ISMAIL
49	AMINA OMARY LIKOKOLA
50	AMINA SALEHE BADI
51	AMON JEREMIA KIHUNDO
52	AMOS YONA RUGALABAMU
53	ANATOLIA COSMAS MAGANGA
54	ANDREW GERALD KITELE
55	ANDREW KIRORI WAGURU
56	ANESI SATOKI MAHENGE
57	ANGELA MOSES MAYEMBA
58	ANITA LUKELO MGOBASA
59	ANNA ALEX HAULE
60	ANNA APOLINARY NDATURU
61	ANNAH ABRAHAM MUSHALA
62	ANNAH KAFULU MWAKIHABA
63	ANNES ANDREA MWALONGO
64	ANNETH BONEVENTURE RWEKAZA
65	ANTHONY ABRAHAM MKWESO
66	ANTIPAS GASPER MZEE
67	APMAEL GIDEON NNKO
68	APOLINARY DEOGRATIAS MINJA
69	ARJANSON MAYNARD MLOGE
70	ASHISH MUKESH JIWAN
71	ASMA SHABANI GENDO
72	ASSAA SIMBA HAROUN
73	ATHUMAN ZUBERI MWESONGO
74	ATHUMANI HAMISI MAGEMBE
75	AURELIA IGNAS KAPINGA
76	AURELIA LAWRENCE LWENZA
77	AVITI JOHN ASSEY

78	AWANJE HEMED MATENDA	123	CHEKA MWAMBUNGU CHAGGE
79	AZIZA ALLY KIMOLO	124	CHEKHA MWAMBUNGU CHAGGE
80	BAHATI ACKSON MWAMAHONJE	125	CHRISTINA LUCAS MATERU
81	BAHATI BYSON MWASIBILA	126	CHRISTINA MALANGWA NGHUMBI
82	BALIYE PHILBERT MISAKAA	127	CHRISTINE NYANJIGA NYAGIRO
83	BARNABAS KASYUPA MWAKIFUNA	128	CHRISTOPHER HENRY KAVISHE(NDEFUNO)
84	BASILISA ANDREW LYIMO	129	CLARENCE ELIHURUMA MAKULE
85	BEATLES GUSTAV LIGAZIO	130	CLAUSI SELEMANI MITWE
86	BELANDO MICHAEL NARDO	131	CLEMENT OBEDIODOM CHANJARIKA
87	BENADINA TENEFAS LYATUU	132	COLETHA KONRAD NTALASHA
88	BENSON LUGOBI NALLYA	133	CONJEPTA THEODORY KESSY
89	BERNADETA WARIOBA CHACHA	134	CONRAD KASIAN NTALASHA
90	BERNADETHA KUVISE MSHANA	135	CONSOLATA HENRY KABUHAYA
91	BERNADETHA PIUS BALLO	136	CONSOLATA JULIUS MUNDEWA
92	BERTHA KIKOTI	137	CONSOLATHA PANTALEO NJAU
93	BETHUEL ELINAJA TEMU	138	CONSTANCIA CASTOR LYARI
94	BISSO SAMSON SENGA	139	CONSTANTINE CHRISTOPHER MSHANGA
95	BLANDINE SAGIRA MONG'ATEKO	140	DAFROZA REMI KIPESHA
96	BONITUS DOMINIC MWALLENI	141	DAINES ELIABU KIMEY
97	BRIGHTON KENAN NDONE ..	142	DAMAS JUMA KAYERA
98	BUJIMU WILLIAM WALWA	143	DAMAS THEOBALD MSAKI
99	BURONGO MATAGE MUSESE	144	Daniel Adolf Olomi
100	CALLISTUS PHILLIP ASSENGA	145	DANIEL GODFREY MANDARI
101	CAMILIUS MATHEO HAULE	146	DANIEL JOSHUA MGEYEKWA
102	CARLTON JERAM BHANA	147	DANIEL MASALU MAGELANI
103	CASSIAN THADEI MBELEKWA	148	DASTO CHAULA MWAKABANA
104	Catherine Francis Tarimo	149	DATIVA AUGUST MALLE
105	CATHERINE GERALD SHONI	150	DAUDI GEORGE KASANGA
106	CATHERINE JACOB BAYNIT	151	DAUDI HEMEDI MBAGA
107	CATHERINE LINUS LYAKURWA	152	DAVID ANGELO MAGEMBE
108	CECILIA NEEMA MUSHOBBOZI	153	DAVID MWAMBOLA KIKUMBULU
109	CECILIA NEEMA MUSHOBBOZI	154	DAVID RAPHAEL MBUMILA ..
110	CELESTINA NEOPHITUS MEGABE	155	DAVID WILLIAM MAKOKO
111	CESILIA SIMON TEMBA	156	DEBORA PHILIP RIOBA
112	CHALO MARCO KALLUNDE	157	DEBORA ZACHARIA KILELE
113	CHARLES IBRAHIM AMAS	158	DELPHINA MALEMI HENRY
114	CHARLES JAMES MIHO	159	DENNIS SIRITO MAKOI
115	CHARLES JONAS LIGONJA	160	DEVIS BARA SIMBILA
116	CHARLES MAPUMO MASUNZU	161	DIDAS JOHN SHIRIMA
117	CHARLES MORRIS KAGOMA	162	DINA HAMUD SAID
118	CHARLES MUTALEMWA TIBEKEBUKA	163	DINA KYUNGAI MANYANGU
119	CHARLES PATRICK MANDAWA	164	DISMAS RAPHAEL NTABINDI
120	CHARLES WAKIHOBI WAMBURA	165	DONALD KAJEGELA MWAKABAGA
121	CHARLES YOHANES KIPANGULA	166	DONALD WARIOBA KISURI
122	CHARLESS BINAMUNGU MUBI	167	DOTTO MHULI

168	DUNCAN LAMECK MUSHI
169	DUNSTAN SEM KISANGA
170	ECKLIAH MICHAEL MBAIGWA
171	EDMUND DANIEL MHALILA
172	EDNA SARAH MSUMBA
173	EDWARD CHARLES HAULE
174	EDWARD DIDAS MIKINA
175	EDWARD WILLIAM BUPILIPILI
176	EDWIN PAUL MUNGA
177	ELIAS MADUHU MANJECHE
178	ELIAS MASANJA MATANGWA (Rep. Jessica Swai)
179	ELIREHEMA NITWA MSEMEMBO
180	ELISAMEHE FESTO URIO
181	ELISANTE ALEWINGYO ULOMI
182	ELISHA BAHATI MWAMAHONJE
183	ELIZABETH DOSLA GEAY
184	ELIZABETH MANSUETUS MOSOI
185	ELIZABETH MARTIN MBOTTO
186	ELIZABETH MOSTA MUSA
187	ELIZABETH ZEBEDAYO MARUWA
188	ELWARDA DEODATUS MGENDELA
189	EMILIA UHAGILE MPESSA
190	EMILLY JAMESI MCHOMVU
191	EMMANUEL JOSEPH DAFTARI
192	EMMANUEL KASALLA TARO
193	EMMANUEL SALULYA MAGUBU
194	ENESTINE HANSON RINGO
195	ENOCK KATABANYA MPAMWA
196	ERASTO BAYNETH CHIWANGA
197	ERASTO MICHAEL GWIMILE
198	ERNEST ISMAEL MTEI
199	ESTA JAMES SHITINDI
200	ESTHER ELIASA BIRANGO
201	ESTHER KAWOGO LIVOGA
202	ESTHER MAULIDI MDENYE
203	ESTOMIHI MOSES MWEMI
204	ESTRIDA JULIUS MGANGA
205	EUPHRASIA GASPAR FUNDI
206	EVA ALOYCE MMBANDO
207	EVA EDWIN LYATUU
208	EVARIST ISDORY MAHOLI
209	EVETTA DION MSELLE
210	EVLASTUS JOSEPH KILUSUNGU
211	FADHIL SALUM WAHID
212	FARIDU IDDI SUNGURA
213	FATMA OMARI ABDULLAH
214	FATUMA ABDALLAH HAULE
215	FATUMA ABDULRAHMAN HIJAH
216	FATUMA RAMADHAN MWAMBA
217	FATUMA SAID BANKA
218	FAUSTER JEREMIAS KIBONDE
219	FELISTER RUWAICHI MOSHI
220	FELIX MICHAEL MUSHI
221	FLAVIA DAMAS KWAI
222	FLORA PETER
223	FLORENCE DENNIS GWANG'OMBE
224	FLORENCE GOODLUCK MLAKI
225	FLORENCE GOODLUCK MLAKI
226	FRANCE PETER TARIMO
227	FRANCIS JOSEPH COSMAS
228	FRANCIS MOHAMED LYAKI
229	FRANCIS Ruzibiza KAMBAYA
230	FRANCIS VICENT MROSO
231	FRANCISCA JOSEPH NGALO
232	FRANK MUWINGU ULIZA
233	FREDERICK TLUWAY SUMAYE
234	FREDRICK ERNEST GUNGAYENA
235	Fredrick Richard Massawe
236	FRIDA STEFANO HAULE
237	FRIDAH LEBI MWAKIPOSA
238	GABBY DANIEL MWASUNGA
239	GAMALIEL JOSEPH KAVIT
240	GARLUS GREGORY MILLANZI
241	GASPAR MICHAEL FUNDI
242	GASPAR MICHAEL FUNDI
243	GASPER JULIUS SHAO
244	GASPER MATHIAS MASINGO
245	GAUDENCE JOHN TARIMO
246	GENEROSE MKANDARA KAMARA
247	GEOFREY MELKIORY MWINUKA
248	GEORGE CALISTUS MAHOMBO
249	GEORGE CLEOPA MAPUNJO
250	GEORGE EDWARD MWAKABANA
251	GEORGE JOSEPH KITUNDU
252	GEORGE MICHAEL LUOGA
253	GEORGE SAMWEL MAGONGO
254	GEORGINER DANIEL BAKALEMWA
255	GERALD EVARIST NJIMBA
256	GERALD JOHN SHOYI

257	GERALDINE KOKWENDA MWIJAGE
258	GERAZIUS ADRIANO KAHAMBA
259	GERVAS JOSEPH KAVISHE
260	GIDEON KELVIN KAZIMOTO
261	GILBERT ALFRED BIGILIMANA
262	GIVENESS IGNAS LWAVI
263	GLADNESS MUKEMFURA RWEJUMURA
264	GLORY JOSEPH ANDREW
265	GODBLESS GIBSON MINJA
266	Godebertha Siima Gonzaga
267	GODLOVE ALFRED NASSARY
268	GODWIN RWEIKIZA RUBAGUMYA
269	GOLDER ANAEL KIMARO
270	GRACE ELINEEMA NABURI
271	GRACE HILARY MBIRIGENDA
272	GRACE LUKINDO
273	GRACE MAMNGODO MAZENGO
274	GRACE MANASE OKORE
275	GRACE MARCO MKINGA
276	GRACE STEVEN KAZOKA
277	GRACE ZACHARIUS KAMONGA
278	GRACEANA RIMISHO SHIRIMA
279	GWERINO RAPHAEL KANGALAWE
280	HABIBA SALUMU YUSUPH
281	HADIJA SALIMU MKINI
282	HAJI RASHID MACHETA
283	HALFAN LIKUKULYUNDU KIHAMBWE
284	HALFEN HALFEN RASHID
285	HALIMA ABDALLAH MOHAMED
286	HALIMA JUMANNE IDDI
287	HALIMA SALIM MWAKING'INDA
288	HALLIMMA MWINYIJUMA MWINYIAMANI
289	HAMIDA ADAM LASHIKONI
290	HAMZA MUNJU ISSA
291	HAPPINESS JOHN BUTOTO
292	HAPPYNES BHOKE MOGASA
293	HARIETH HERMENEGILD SWAI
294	HARUNA ZUBERI MSATI
295	HASHIEM HEMED MAHSOUDH
296	HASHIMU RAMADHANI MUSHI
297	HASSAN HAJI MKINDWA
298	HASSANI ATHUMAN MPAMBIJE
299	HELLEN SIMON MAZANI
300	HENED AIDHA FEREJI
301	HENRY AUGUSTINO NYANSWE
302	HENRY BATHOLEMEW MWAKIBETE
303	Herieth Samson Kabuje
304	HERIETH KAIJAGE KIPARA
305	HIDAYA NDEVUMBILI HAMISI
306	HILARIOUS SIMONI KAMUGISHA
307	HILDA AUGUST LYIMO
308	HILDA LAZARO
309	HILDA MASWA MUHAVI
310	HILDA NICHOLAS MKALA
311	HILDER CONNIE MATOVU
312	HUSNA RUMISHA MAKUNDI
313	HUSSEIN BAKARI KINGUYU
314	HYASINTA JOHN TEMBA
315	IBRAHIM MASUDI NZOWAH
316	IBRAHIM MUSSA LUTHER
317	IBRAHIM PHILIP LESSAFI
318	IBRAHIM YUSUFU MALUNGUMO
319	IGNACE DAMAS MBUNJU
320	IGNAS VANGACHUMA MLWALE
321	INNOCENT MARTIN SHIRIMA
322	INNOCENT NORASCO SANGA
323	INVOCATH ALEONANSIA MUNUO
324	INYASI KILAIDI SHIRIMA
325	IRENE CHARLES KAMUGISHA
326	IRENE COSTANTINE MTOBESYA
327	IRENE FRANCIS FUGARA
328	IRENE MKASHIDA MSAFIRI
329	ISABELLA HUSSEIN KAPER
330	ISRAEL DAUDI NGANDO
331	IWIRINAMSO JOHN MANASE
332	JACOB SYLVESTER MACHIYA
333	JACQUELINE INNOCENT NJOVU
334	JAIROS YAHYA FWIMI
335	JAMES EMMANUEL CHINGUKU
336	JAMES JOSEPH MAKUNDI
337	JAMES WANGALUKE MANYANGU
338	JANE EMMANUEL MOLLEL
339	JANE JAMES MWAMELE
340	JANE NKULANGOWE AGWANDA
341	JANE SIMON TATALA
342	JANET SAMWELI KIVUYO
343	JANETH GODWIN KYAMBA
344	JANETH MAYA
345	JANUARY MTUMWA MASUDI
346	JASMEEN BENJAMIN KIHELE


347	JASTONE HULEGE KABONA
348	JAYANT PREMJI VAGHELA
349	JESSICA ERNEST SWAI
350	JOANITHA KOKU MABULA
351	JOEL FURAHA MUSHI
352	JOHANNES CLEMENCE MUTAHYOBIA
353	JOHN DAMAS KAGERE
354	JOHN PRISCUS SYLIVESTER
355	JOHNY ENOCK MWAKATOVE
356	JONATHAN ATUPELE MWABALEKE
357	JONESIA NEOPHITUS MEGABE
358	JOSEPH ANTHONY KULIJA
359	JOSEPH CHARLES BUNDALA
360	JOSEPH KISMAYU KISARIKA
361	JOSEPH SOLOMON KITUNDU
362	JOSEPH SUTING KAWICHE
363	JOSEPHAT PETIN MSHAMA
364	JOSHUA ATHANASIUS MWANZA
365	JOSHUA WILLIAM KANIKI
366	JOSHUA ZAKAYO KICHAO
367	JOYCE JOHN MOSHI
368	JOYCE JOSEPH KITUNDU
369	JOYCE SOLOMON SAMWEL
370	JUANITA SIE PUJA
371	JUBILATE BERNARD MINJA
372	JUDAS ATHUMANI MRUTU
373	JUDITH PANTELEO NJAU
374	JUDITH PAULO LUANDA
375	JULIA JOSEPH TARIMO
376	JULIET JONAS MWAKALUKWA
377	Julieth James Kajugusi
378	JULIETH STEPHEN SHAYO
379	JULITHA ELIREHEMA MARANDU
380	JULIUS ENOS JOHNAS
381	JULIUS LIKAVANGA MAGODA
382	JUMAA MUSSA HIZZA
383	JUMAPILI ABDALLAH KHALIKI
384	JUSTIN JAMES GWASE
385	KALUNDE WILSON KASELE
386	KAMBETTA ANDREAS MWINUKA
387	KARANGI BERNARD BWIRE
388	KASIM MUSSA HAMISI
389	KAUNDA ARTHUR MWANYANJE
390	KEFA MELKIZEDECK MHAPA
391	KENEDY EDWARD MWALUKASA - -
392	KENNEDY KIMANDAI LYIMO
393	KHADIJA MIKIDADI SENKONDIO
394	KHASHIR SEIF SAID
395	KHOZAIF SADIK MERALI
396	KILLENGA MANSUETH MOSOI
397	KULWA SAIDI MDULA
398	KURUTHUM AHMED SAMULI
399	KYANG'A AWWAM UMBA
400	LADSLAUS METHEW MAKENZI
401	LATIFA RAMADHANI BIRO . .
402	LAZARUS PETER MPONDO
403	LEOCADIA PANTALEO NJAU
404	LEOCADIA THOBIAS SIWEYA
405	LEOGRAVE FERDINANDES MSOMA
406	LEONARD JOHN MIDELO
407	LEONARD JOHN MIDELO
408	LEONTIA IBIKA RWECHUNGURA
409	LEVINA MARTIN MAX-MILLIAN
410	LILIAN KOKUSHERULA NYOMBI
411	LILIAN PETER MASELE
412	LILIAN ZEBEDAYO RIWA
413	LINUS ALOYCE NGOWI
414	LISSU SHABAN LISSU
415	LOIRUCK JONATHAN MOLLEL
416	LUCAS SALAMA KYUNGU
417	LUCIANA DANIEL THONYA
418	LUCIUS OTMARY MLELWA
419	LUCY CHARLES MAMBALI
420	LUCY GOZIBERT MUTAHYABARWA
421	LUDAN FABIANI TARIMO
422	LUSUBILO FREDRICK MALAKBUNGU
423	LYDIA KARIKIA MUNUO
424	LYDIA LUDOVICKY MUTALEMWIA
425	LYISON THOMAS KALULUNGA
426	MAGDALENA MUSHI MSAFIRI
427	MAGDALENA SELESTINE KUSYAMA
428	MAHEKE JOSEPH MAHEKE
429	MAJALIWA TAMBALA NGONJI
430	MAJID SEIF SAID
431	MALEGERI MASHAURI LUCAS
432	MALIKI MASAMBAJI DAUDI
433	MAOVU HATIBU ALLI
434	MARGARETH JOSEPH SHILLAH
435	MARGARETH NGELULA NATHANIEL
436	MARGERATH HEBRON MWAIPAJA

437	MARIA GORETTI KENTE
438	MARIA SIMON MWAGALA
439	MARIAM DANIEL SOZIGWA
440	MARIAM EMILIAS FUSI
441	MARIAM HAMISI MWANGIA
442	MARIAM MASOUD MAHUGU
443	MARIANUS GERVAS MWANGAMILA
444	MARIDHAWA HOJAJI SAID
445	MARIETHA EDWARD LYIMO
446	MARIETHA JOHN CHANDE
447	MARTIN FRIMOS MSELLE
448	MARTIN JONAS MMARI
449	MARTIN RAPHAEL SIWINGWA
450	MARY DANIEL OBANGA
451	MARY GEORGE LUSWAGA
452	MARY JEREMIAH MWANYANJE
453	MARY JOHNSON RUHASHA
454	MARY KOKA LEWANGA
455	MARY MELKIORY MNYAWAMI
456	MARY RAIMOND LUAMBANDO
457	MARYSTELLA AUGUST MALLE
458	MASHAURI KALIWA KALIMU
459	MATHEW PETER NYASA
460	MATHIAS JOHN MUSHI
461	MATILDA KOBELO VITUS
462	MEING'ARAI LUKUMAY MEJOLLY
463	MERCY ALBERT MMARI
464	MERCY BERNARD MPANGALA
465	MERCYANA THOMAS BUNONU
466	MERIKA LEONARD MAGODA
467	MHAMADI UMALI MBELWA
468	MICHAEL JOHANESS MWITA
469	MICHAEL MHANDO KILLO
470	MICHAEL ZAKARIA MATTEE
471	MICHAELA LADISLAUS LIHEPANYAMA
472	MINNIE ELIAPENDA LEMA
473	MIRIAM BERNAD MMBAGA
474	Miriam Mickson Wales
475	MKIWA NASSORO MWINYI
476	MKUMBO EDSONI MSENGI
477	MKUNGURA HASHIM MKUNGURA
478	MODEST ADRIAN ZONGEYE
479	MODESTER FRANCIS FUMBUKA
480	MOHAMED MTENYA MAKINDI
481	MOHAMED SALUM MAKILIKI
482	MOHAMED HASSAN MFAUME
483	MOHAMMED RAMADHANI NGUDE
484	MOHEMED AHMED MOHEMED
485	MOSES ANDREW MAHENGE
486	MOSES ELIAS ALOYCE
487	MOURINE HAPPYGOD MOLLEL
488	MRS WILFRIDA ALOYCE MALLYA
489	MRUMA SULEIMANI MRUMA
490	MTAHETWA KULWA LUBOLA
491	MTUMWA SAID MOHAMED
492	MUSSA MASUDI MFAUME
493	MUSTAFA JAMADI SILIMA
494	MUSTAFA KOMBO OMARY
495	MWAJUMA RASHIDI BUNGA
496	MWANAHAMIS SULTAN KAWA
497	MWANAHAWA BAKARI HADINGOKA
498	MWANAMWEMA KAHMIS MLINDO
499	MWANEEMA MWINYIJUMA MWINYIAMANI
500	MWANJAA JUMA MAGEE
501	MWINYIAMANI MWINYIJUMA MWINYIAMANI
502	MWINYIJUMA MIKIDADI MWINYIAMANI
503	MZEE MANGUPIRU MANDAWA
504	NAIMA ATHUMANI KATUNZI
505	Najim Babu Rashid
506	NANCY DAVID MSOBI
507	Naomi Hezron Lutumo
508	NAPENDAELI WAZOELI NYARILA
509	NARCISA NYONI MUNG'ONG'O
510	NATHANIEL RAJABU MBWAMBO
511	NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
512	NDENI ANANDE SHOO
513	NECTA MAWALLA RAYMOND
514	NEEMA MELCHIOR NUNGU
515	NELSON ELIA KIWELU
516	NEZIA PETER GAINI
517	NGALAI LEONS NGALAI
518	NHC AND PPF INVESTMENT CO. LTD
519	NICHOLAUS CHARLES BUNDALA
520	NICHOLAUS MALANDO GREGORY
521	NICHOLAUS STANISLAUS LYIMO
522	NICODEMUS TUSEKELEGE MWASIKILI
523	NOAH JORAM NZAWILA
524	NOBERT SHIRIMA
525	NOEL SIMON TEMU
526	NOOR RAJABU KITETEY

527	NURU SENGO MSENGWA
528	NYAKIMURA MATHIAS MUHOJI
529	NYAMAGELO ZACHARIA MAKUBI
530	NYANJURA REUBEN NYARUGA
531	OBEID ABDALLAH HAULE
532	OMARI HUSSEIN BORI
533	ONESMO RICHARD NDAKI ..
534	PAL MORICE KAMKANILA
535	PANDE NDEGEYA KIZINGA
536	PARASTATAL PENSION FUND (PPF)
537	PARASTATAL PENSIONS FUND
538	PASKAZIA JOHN BULIMBA
539	PASTORY CHARLES NYANDA
540	PASTORY MUYONGA NGAIZA
541	PATRICIA GERALD MWAISENDOLA
542	PATRICK MTATIRO CHEGERE
543	PAUL WILBARD LUANDA
544	PAULINA CALIST KISHAI
545	PELAGI LEFUNGONI WOISO
546	PELAGI LEFUNGONI WOISO
547	PETER ASAGWILE MWASONGWE
548	PETER ISHENGOMA MUGANYIZI
549	PHILEMON AIDAN MKONY
550	PHILEMON ALLAN MSUYA
551	PHILLIP JAMES MGONJA
552	PILLY ANASTASIUS NGAPEMBA
553	PIUS PHILILIP TESHA
554	PIUS PHILLIP TESHA
555	PRISCILLA MUKABALUZI RWEYEMAMU
556	PRIVATUS JOHN MUTASHOBYA
557	PROCOPIUS EMMANUEL MGIMBA
558	RAHELI OMARI KATOYA
559	RAHILU IDDI NYUNDO
560	RAJABU ABDALLAH FARAHANI
561	RAJABU IBRAHIM MSUMI
562	RAJABU RAMADHANI LUKENZE
563	RAJABU SHAMTE MKELEKA
564	RAMADHANI ALLY SEIF
